


HAKI ZA URAIA NCHINI KENYA




Imetayarishwa kwa ushirikiano na:

 Haki na Sheria



 OPEN SOCIETY
FOUNDATIONS

Kipengele cha 15 katika azimio la ulimwengu juu ya haki za binadamu kinasema kuwa:
Kila mtu anahaki ya kuwa raia na kuwa hakuna atakayenyimwa uraia kiholela au kunyimwa haki ya kubadilisha uraia wake



Ni nani ambaye ni raia au anaweza kuwa raia wa Kenya ?




Mtu anaweza kuwa raia wa Kenya kupitia njia moja kati ya hizi mbili:

1) Kwa kuzaliwa , almuradi:

i). Amezaliwa nchini Kenya baada ya Desemba 11,1963, →
na

Katiba
Schedule 6,
Article 30

ii). Mmoja wapo wa wazazi wake(kipindi anachozaliwa)
ni raia wa Kenya



2) 2) Kujisajili serekalini kwa mambo haya yafwatayo:

i) Kuolewa na mkenya (kwa miaka isiyopungua saba) →

Citizen &
immigrations act
Section 15(1)

ii) Kuishi Kenya kihalali. →

Section 15(2)

iii) Kutwaa/kupanga (adopt) (mtoto asiyekuwa
mkenya na raia wa Kenya) →

Section 15(3)

iv) Mtu asiyekuwa na uraia. →

Section 15

v) Mhamiaji (ikiwa ni mkaazi wa Kenya
kufikia mwaka wa 1963) →


Section 16

vi) Kuwa mtoto wa wasiokuwa na uraia au wahamiaji
ambao wametosheleza matakwa ya usajili →

Section 17

Ni mambo yapi ninayostahiki kama raia wa Kenya?

Kulingana na katiba ya Kenya ,2010, raia wote wanastahiki:



- Haki ya Kupiga kura
- Paspoti ya Kenya na stakabadhi yeyote nyengine ya usajili au utambulisho inayotolewa na taifa kwa raia.
- Haki ya kupata elimu ya msingi
- Fadhila kama vile malipo ya wazee au wajane



Je serekali inaweza kuninyima stakabadhi za kujitambulisha?

- Ikiwa wewe ni raia, unaweza kunyimwa paspoti au stakabadhi nyengine yoyote, kusitisha matumizi yake au kunyang'anywa stakabadhi hizo pale tu utakapo timiza matakwa yaliyotajwa na mswada wa bunge yenye kutimiza vigezo vilivytajwa katika sura ya 24



Sura 24.

Je kunazo sheria za kimataifa zenyenye kulinda haki zangu za kupata uraia ?

Sheria nyingi za kimataifa zinasisitiza kuwa kila mtu anahaki ya uraia (hujulikana pia kama uwana-nchi). Kwa mfano:

- Mkataba wa kumaliza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW). Kipengele cha 91. Wan awake watakuwa na haki sawa na wanaume, kutwaa au kubadilisha au kudumisha uraia wao.
- Mkataba wa haki za watoto. Kipengele cha 71. Mtoto atasajiliwa punde tu baada ya kuzaliwa na atakuwa na haki ya kupewa jina, hakii ya kutwaa uraia na kadri iwezekanavyo haki ya kuwajua na kulelewa na wazazi wake.
- Azimio la ulimwengu juu ya haki za binadamu, kipengele cha 15.
 - Kila mtu anahaki yakuwa raia
 - Hakuna atakayenyimwa kiholela uraia wake
 - Kila mtu anahaki kubadilisha utaifa wake.

Ni kwanini mtoto wangu anahitajia cheti cha kuzaliwa?



Ni kwanini mtoto wangu anahitajia cheti cha kuzaliwa ?

Mtoto wako anahitajia cheti cha kuzaliwa ili:

1. Kujisajili shule ya chekechea, shule ya msingi na shule ya sekondari
2. Kuweza kuingia katika hospitali za kibinafsi ili kupata matibabu
3. Kujisajili kufanya mtihani wa mwisho wa shule ya msingi
4. Kufanya maombi ya kitambulisho anapohitimu miaka kumi na minane
5. Kufanya maombi ya paspoti na pia paspoti za watoto wao
6. Kujisajili katika NSSF


HATUA ZA KUSAJILI

HATUA 1



Hakikisha una stakabadhi hizi
 -Kadi halisi ya notification
 -Nakala (copy) ya notification (hii ni karatasi ya rangi ya waridi(pink) unayopewa pale hospitalini baada ya motto kuzaliwa)
 -Nakala (copy) ya kitambulisho cha baba
 -Nakala ya kitambulisho cha mama
 -Copy ya kadi ya kliniki

HATUA 2



Tembelea ofisi ya msajili wa vifo na mazazi wa wilaya, utapewa fomu ili ujaze.

HATUA 3



Ambatanisha fomu hiyo na nakala za vitambulisho na karatasi ya notification kisha umrudishie msajili .

HATUA 4



Maelezo uliyoyatoa ya-tahakikisha kisha utumwe kwa keshia ili kulipia

HATUA 5




Lipa kiwango kinachohitajika katika ofisi ya usajili wa mazazi:
 Ada ya maombi haipungui shilingi 50 na haizidi shilingi 150

HATUA 6



Utapewa risiti utaka-yoitumia kuchukulia cheti chako. Cheti kitakuwa tayari baada ya wiki mbili.

Ni kwanini nahitajia kitambulisho ?



Ni kwanini nahitajia kitambulisho ?
Mtu yeyote mwenye umri uliozidi miaka kumi na nane anahitajia kuwa na kitambulisho

1. Ili Kujisajili chuo kikuu
2. Ili Kupata kazi
3. Ili Kusajili laini ya simu na Televisheni
4. Ili Kuipa nguvu ombi la paspoti
5. Ili Kununua ardhi na mali nyengine kama vile gari.
6. Ili kupata pin number yako ya kulipia ushuru.
7. Ili kuingia katika majengo
8. Ili Kujisajili kama mpiga kura na kupiga kura

Kitambulisho cha kitaifa ndicho stakabadhi halali cha utambulisho kinachotambuliwa nchini Kenya.

HATUA ZA KUSAJILI

1

1. Chukua stakabadhi zifuatazo na uje nazo katika ofisi ya msajili wa wilaya.
- Cheti chako halisi cha kuzaliwa
 - Nakala (copy) ya cheti chako halisi cha kuzaliwa.
 - Cheti chako cha kumaliza shule (ikiwa unacho)
 - Vitambulisho halisi vya wazazi wawili
 - Nakala(copy) ya vitambulisho vya wazazi wawili.



2

Mpeleke stakabadhi hizo msajili wa wilaya ili upate kitambulisho cha taifa. Jaza fomu bila makosa yoyote. Kisha fomu ulioijaza kwa chifu au naibu wake ili itiwe sahihi.

3

Peleka fomu zilizotiwa sahihi katika ofisi ya msajili wa wilaya, amabako maelezo ulioandika yatahakikishwa kisha Yule msajili atatia sahihi katika ile fomu.ukishamaliza hatua hii alama zako za vidole zitachukuliwa kisha upigwe picha ya paspoti ambayo itaambatanishwa pamoja na fomu na kutumwa katika ofisi za kuundia vitambulisho.

4



Utapewa kadi ya kusubiria ambayo utaitumia kipindi ambacho unasubiria kitambulisho chako kitengenezwe. Muda wa kusubiria huenda ukafika hata mwaka mmoja.

5

Baada ya miezi miwili nenda katika ofisi ya msajili ili kuangalia uwepo wa kitambulisho chako. Kumbuka kuwa inaweza kuchukua muda wa mwaka mmoja ili kupata kitambulisho chako. Kwahivyo Itakulazimu kucheki mara baada ya nyengine.



Ninawezaje kupata paspoti?



Jinsi ya Kujisajili

Mkenya ye yeye mwenye nia ya kuchukua au kusafiri nje ya nchi atatakiwa kuwa ni mwenye kufanya maombi yake ye yeye binafsi kwa ofisa mhusika kwa njia inayostahiki. Karatasi za usajili zinaweza kuwasilishwa katika ofisi za PASSPORT CONTROL Nairobi, Mombasa au Kisumu .

HATUA ZA KUSAJILI

1



Fungua tovuti ya ecitizen.go.ke kisha fungua akaunti. ingia kwenye akaunti baada ya usajili kisha nenda katika kitengo cha huduma za uhamiaji (Department of immigration services) kisha wasilisha ombi (Submit application) kisha paspoti na pasi za muda (Passport and temporary permits)

2



Unatakiwa kubofya palipoandikwa "Passport Application form" ukurasa utakao funguka una maagizo ya jinsi ya kujaza fomu ya maombi. baada ya kusoma maagizo teremka chini kisha bofya hapo palipoandikwa "APPLY NOW" Jaza fomu ya maombi

5

Chukua paspoti yako kwa muda usiopungua siku kumi za kazi



- Peleka fomu yako mwenyewe pamoja na stakabadhi takiwa katika ofisi ya immigration ilioko karibu nawe.
- Unatakiwa kuwa na fomu uliyojaza. copy mbili za risiti kuonesha malipo. kitambulisho chako pamoja na copy yake, cheti chako cha kuzaliwa pamoja na copy yake, copy cha kitambulisho cha aliyeupendekeza (recomender). picha tatu za paspoti na copy za vitambulisho vya wazazi wote wawili. ikiwa wazazi wamefariki utatakiwa kuwa na copy za vyeti vyao vya kifo.
- Peleka fomu yako Nyayo house.

4

3




Chagua jinsi ya malipo kisha lipa ada ya paspoti

Unaweza kulipa kuitia: M-PESA, Debit/Credit card, Airtel money na eCitizen Agent.

Pakua(download) kisha chapisha(print) fomu za maombi na risiti tatu za usajili




KWA NINI NAHITAJIA VYETI VYA KIFO?



Utahitajia cheti cha kifo cha mchumba wako, wazazi au mtu wa familia yako

- Kuipa nguvu ombi la mtu ambae wazazi wake wamefariki
- Kuagiza urithi.
- Kubadilisha umiliki wa gari au mali kwa majina yao

HATUA ZA KUSAJILI





SHUKRAN



P.O. Box 22677-00505 Nairobi.
www.namati.org